# Kujenga Mistakabali Bora

ATTENDANCE MATTERS RI COOL2SCHOOL


Mwaka wa masomo unavyoendelea, tungependa kutoa shukrani zetu kwa usaidizi na ushiriki wako endelevu katika elimu ya mtoto wako. Tunaamini kwamba kila mtoto anastahili kupata elimu bora inayomtayarisha kwa mustakabali bora. Kuanzia kozi zinazofaa za kutimiza mahitaji halisi hadi fursa za kipekee na zinazovutia za kujifunza nje ya shule, Rhode Island inashughulika ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata wanachohitaji ili kufanikiwa wakati wa safari yao ya kielimu na kuhitimu wakiwa tayari kwa chuo na kazi. **Tafadhali kumbuka kuwa kuwepo ni muhimu ili wanafunzi kujifunza. Rhode Island inafafanua utoro wa muda mrefu kama asilimia ya wanafunzi ambao hukosa kuhudhuria 10% au zaidi ya siku za shule wakati wa mwaka (au siku mbili kwa mwezi).**

**Siku 18** humfanya mtoto wako kuwa mtoro kwa muda mrefu.
**Siku 10** humweka mtoto wako hatarini.

***Mtoto wako amekosa kuhudhuria siku ngapi za mafundisho?***

Kuna tofauti kubwa katika matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wanaokosa kuhudhuria shule kwa muda mrefu, kama inavyoonekana katika data iliyo hapa chini:

**Asilimia ya Ujuzi Katika Mwaka wa 2024: Wanafunzi Wanaokosa Kuhudhuria Shule kwa Muda Mrefu Wakilinganishwa na Wanafunzi Wasiokosa Kuhudhuria Shule kwa Muda Mrefu**




## Kwa nini ni muhimu?

Watoto wanaokosa kuhudhuria shule kwa muda mrefu wakati wa chekechea na darasa la kwanza wana uwezekano mdogo wa kuweza kusoma kwa kiwango kinachotarajiwa kwa darasa kufikia darasa la tatu.

Utoro wa muda mrefu ndicho kiashiria kimoja kikuu zaidi cha kuacha shule kabla ya kuhitimu.

Wanafunzi wanaoacha shule wana uwezekano mdogo wa kufanikiwa kazini. Kwa kweli, mtu aliyehitimu kutoka katika shule ya upili kwa wastani hupata dola milioni moja zaidi kuliko mwanafunzi aliyeacha shule katika maisha yake yote.

Utoro wa muda mrefu unahusishwa na ongezeko la matukio ya kusimamishwa kuhudhuria shule kwa muda, matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana, pamoja na afya mbaya wanapokuwa watu wazima.

85% ya wanafunzi wanaoacha shule ya upili walikuwa watoro kwa muda mrefu. Jambo hili linaweza kutabiriwa mapema kama kufikia darasa la tatu, kulingana na mahudhurio yao ya mwanzoni katika shule ya msingi.

**www.ride.ri.gov | www.attendancemattersri.org**



# RICAS ya Majira ya Kuchipua ya 2025 Ripoti ya Mwanafunzi Binafsi

RIDE Rhode Island Department of Education

| | |
|---|---|
| **Jina:** | **Wilaya:** |
| **SASID:** | **Shule:** |
| **Tarehe ya Kuzaliwa:** | **Darasa:** |

Ripoti hii inatoa matokeo ya mtoto wako katika mitihani ya 2025 ya Mfumo wa Tathmini ya Kina wa Rhode Island (RICAS) katika Sanaa ya Lugha ya Kiingereza (kusoma na kuandika) na hisabati.

Taarifa kutoka RICAS pamoja na tathmini nyingine za kielimu na kijamii, zitawasaidia walimu kutathmini uwekaji wa kiwango cha darasa, kubuni mafundisho maalum, kuweka malengo ya kujifunza na kufuatilia maendeleo. Mitihani hii itawezesha shule, wilaya na RIDE kutambua maeneo tunayohitaji kuchukua hatua ili kuboresha ufundishaji na kujifunza. Kila mwanafunzi anastahili kupata nafasi sawa ya kuonyesha anachoelewa, na RIDE inatoa shukrani zake kwa wafanyakazi wetu wa shule ambao huendesha mitihani na wanafunzi ambao huonyesha wanachojua wakati wa mitihani ya RICAS kila mwaka.

Tunakushukuru kwa ushiriki wako katika mitihani hii ambayo husaidia kuelekeza kazi muhimu ya kuboresha matokeo ya wanafunzi. Tunatumai kuwa kuelewa ufahamu wa mtoto wako wa ELA na maarifa na ujuzi wa hisabati kutakuwezesha zaidi unapomtetea mtoto wako. Unamjua mtoto wako vyema zaidi. Kwa taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kuelewa matokeo, tembelea www.RIDE.ri.gov/Assessment-Results.

**Kwa kila somo, ripoti inaonyesha:**

- Alama za mtoto wako kati ya 440 na 560 na kiwango chake cha mafanikio
- Jinsi mtoto wako alivyofanya katika kusoma na hisabati kulingana na kategoria za kuripoti za mtihani
- Alama ya kuimarika ambayo inaonyesha jinsi mtoto wako alivyofanya akilinganishwa na wanafunzi wengine waliopata alama sawa

## Matokeo ya Jumla ya Mtoto Wako

| Sanaa ya Lugha ya Kiingereza | Hisabati |
|---|---|
| Kiwango cha Mafanikio | Kiwango cha Mafanikio |
| Alama | Alama |
| (Kiwango cha alama: 440–560) | (Kiwango cha alama: 440–560) |
| Asilimia ya Kuimarika | Asilimia ya Kuimarika |
| **Maelezo yapo kwenye ukurasa wa 2** | **Maelezo yapo kwenye ukurasa wa 3** |

**Je, ulijua kwamba kuanzisha mazoea ya familia kunaweza kumsaidia mtoto wako kufaulu?**
Anzisha mazoea ya kutenga nyakati maalum za kufanya kazi za nyumbani, kusoma, nyakati za kula, mazungumzo ya familia, wakati wa kulala na kuondoka kwenda shuleni kila siku.

**Nifanye nini baadaye?**
Baada ya kupitia ripoti hii, ni muhimu uhudhurie mikutano ya walimu na familia na kujadiliana na walimu wa mtoto wako kuhusu maswali na wasiwasi wako. Usiogope kuongea. Watoto ambao familia zao husisitiza umuhimu wa elimu wana uwezekano zaidi wa kuiona kuwa muhimu pia.

**Ninawezaje kuunga mkono elimu ya mtoto wangu?**

- Kuhudhuria shule ni muhimu, kila siku. Kukosa kuhudhuria shule kwa siku mbili tu kwa mwezi kunamaanisha kwamba mwanafunzi wako ni mtoro kwa muda mrefu. Kwa hivyo, hakikisha unaweka umuhimu wa kwanza wa kumpeleka mtoto wako shuleni kwa wakati unaofaa kila siku.
- Anzisha taratibu za kusoma za kila siku, acha mtoto wako akuone ukisoma na umhimize mtoto wako asome ili kujifurahisha kwa mwaka mzima.
- Jihusishe na uendelee kuungana na shule ya mtoto wako, kwa njia yoyote na wakati wowote unapoweza.
- Shiriki maoni yako! Saidia kuboresha shule ya mtoto wako kwa kushiriki katika SurveyWorks kila mwaka.

Anzisha mazungumzo. Uliza maswali. Zungumza na mtoto wako kuhusu anachojifunza na uonyeshe kuwa unavutiwa na masomo yanayomsisimua. Kumbuka, wewe pia ni mwalimu wa mtoto wako na una jukumu muhimu la kumwandaa mtoto wako kupata mafanikio.

Jina:
SASID:

## Sanaa ya Lugha ya Kiingereza



| | |
|---|---|
| Kiwango cha Mafanikio cha Mtoto Wako: | |
| Alama ya Mtoto Wako: | |

**440** Hatimizi Matarajio **470** Anatimiza Matarajio kwa Kiasi Fulani **500** Anatimiza Matarajio **530** Anazidi Matarajio **560**

**Hatimizi Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki hakutimiza matarajio ya kiwango cha darasa katika somo hili.

Shule, kwa kushauriana na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, inapaswa kubaini usaidizi unaoratibiwa wa kielimu na/au mafundisho ya ziada ambayo mwanafunzi anahitaji ili kufaulu katika somo hili.

**Anatimiza Matarajio kwa Kiasi Fulani:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alitimiza matarajio ya kiwango cha darasa kwa kiasi fulani katika somo hili.

Shule, kwa kushauriana na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, inapaswa kuzingatia iwapo mwanafunzi huyo anahitaji usaidizi wa ziada wa kielimu ili kufaulu katika somo hili.

**Anatimiza Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alitimiza matarajio ya kiwango cha darasa na anafanya vyema kielimu kuelekea kufaulu katika darasa la sasa katika somo hili.

**Anazidi Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alizidi matarajio ya kiwango cha darasa kwa kuonyesha ustadi katika somo hilo.

Mstari mlalo wa kijivu ulioonyeshwa kwenye michoro iliyo hapo juu na chini unaonyesha kiwango cha alama zinazowezekana ambazo mtoto wako angepata iwapo angefanya mtihani mara nyingi.


### Mafanikio

Jinsi mtoto wako alivyofanya akilinganishwa na wanafunzi katika shule, wilaya na jimbo lake.

| Mtoto Wako | | Mwaka | Alama ya Wastani | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Darasa Lake | Alama | | Shule | Wilaya | Jimbo |
| | | 2025 | | | |
| | | 2024 | | | |

### Asilimia za Kuimarika kwa Mwanafunzi katika Mwaka wa 2025

Alama za mtoto wako za mwaka huu zinalingana au ni bora kuliko asilimia ya wanafunzi wa Rhode Island waliopata alama sawa na za mtoto wako kwenye mtihani/mitihani katika mwaka/miaka iliyopita.




### Jinsi mtoto wako alivyofanya katika kila kategoria ya kuripoti na katika kila swali maalum la mtihani

| Kategoria ya Kuripoti | Alama Ambazo Mtoto Wako Alipata | Jumla ya Alama Zinazowezekana | Alama za Wastani: Shule | Alama za Wastani: Wilaya | Alama za Wastani: Jimbo | Alama za Wastani Ambazo Wanafunzi Wanaotimiza Matarajio Walipata |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kusoma | | | | | | |
| Lugha† | | | | | | |
| Kuandika‡ | | | | | | |

† Kategoria ya kuripoti ya Lugha inajumuisha alama za sarufi ya Kiingereza.
‡ Kategoria ya kuripoti ya Kuandika ni ya alama za kukuza wazo.

### Maswali Maalum ya Mtihani

| Nambari ya Swali | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | 32 | 33 | 34 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama Alizopata | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

**Ufafanuzi** x/y = alama x alizopata kati ya alama y zinazowezekana
ID = Alama ya kukuza wazo la insha
Nafasi tupu = hakuna jibu
CV = Alama ya kanuni za uandishi wa insha
N/A = Swali halikutolewa



Jina:
SASID:

## Hisabati



| | |
|---|---|
| Kiwango cha Mafanikio cha Mtoto Wako: | |
| Alama ya Mtoto Wako: | |

**440** Hatimizi Matarajio **470** Anatimiza Matarajio kwa Kiasi Fulani **500** Anatimiza Matarajio **530** Anazidi Matarajio **560**

**Hatimizi Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki hakutimiza matarajio ya kiwango cha darasa katika somo hili.

Shule, kwa kushauriana na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, inapaswa kubaini usaidizi unaoratibiwa wa kielimu na/au mafundisho ya ziada ambayo mwanafunzi anahitaji ili kufaulu katika somo hili.

**Anatimiza Matarajio kwa Kiasi Fulani:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alitimiza matarajio ya kiwango cha darasa kwa kiasi fulani katika somo hili.

Shule, kwa kushauriana na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, inapaswa kuzingatia iwapo mwanafunzi huyo anahitaji usaidizi wa ziada wa kielimu ili kufaulu katika somo hili.

**Anatimiza Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alitimiza matarajio ya kiwango cha darasa na anafanya vyema kielimu kuelekea kufaulu katika darasa la sasa katika somo hili.

**Anazidi Matarajio:** Mwanafunzi aliyepata matokeo ya kiwango hiki alizidi matarajio ya kiwango cha darasa kwa kuonyesha ustadi katika somo hilo.

Mstari mlalo wa kijivu ulioonyeshwa kwenye michoro iliyo hapo juu na chini unaonyesha kiwango cha alama zinazowezekana ambazo mtoto wako angepata iwapo angefanya mtihani mara nyingi.


### Mafanikio

Jinsi mtoto wako alivyofanya akilinganishwa na wanafunzi katika shule, wilaya na jimbo lake.

| Mtoto Wako | | Mwaka | Alama ya Wastani | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Darasa Lake | Alama | | Shule | Wilaya | Jimbo |
| | | 2025 | | | |
| | | 2024 | | | |

### Asilimia za Kuimarika kwa Mwanafunzi katika Mwaka wa 2025

Alama za mtoto wako za mwaka huu zinalingana au ni bora kuliko asilimia ya wanafunzi wa Rhode Island waliopata alama sawa na za mtoto wako kwenye mtihani/mitihani katika mwaka/miaka iliyopita.




### Jinsi mtoto wako alivyofanya katika kila kategoria ya kuripoti na katika kila swali maalum la mtihani

| Kategoria ya Kuripoti | Alama Ambazo Mtoto Wako Alipata | Jumla ya Alama Zinazowezekana | Alama za Wastani: Shule | Alama za Wastani: Wilaya | Alama za Wastani: Jimbo | Alama za Wastani Ambazo Wanafunzi Wanaotimiza Matarajio Walipata |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

### Maswali Maalum ya Mtihani

| Nambari ya Swali | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | 32 | 33 | 34 | 35 | 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama Alizopata | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

**Ufafanuzi** x/y = alama x alizopata kati ya alama y zinazowezekana
Nafasi tupu = hakuna jibu
N/A = Swali halikutolewa